**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**
**SHULE YA SEKONDARI ZANAKI**

S.L.P. 20592
**DAR ES SALAAM**

Kumb.Na.ZSS/F.5/J.1/2025 Tarehe……………………...

**Jina la Mwanafunzi……………………………………………………………………………………………………….**
**Kutoka Shule ya Sekondari**…………………………………………………………………………………………….

**YAH: <u>MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI ZANAKI HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM MWAKA ............</u>**

1.0 Nafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Kidato cha **Tano HKL, EGM, HGK, HGE,HGL, KLF** katika shule ya Sekondari **Zanaki**, mwaka **2025/2026.** Shule hii ipo eneo la Upanga Mashariki Mtaa wa **Kibasila,** Barabara yahospitali ya Regency. Ukitumia usafiri wa basi shuka katika kituo cha basi cha **AKIBA/FIRE**/**BARIDI.**
Muhula wa kuanza masomo utaanza tutakapotangaziwa. Utatakiwa kuripoti shuleni bila kukosa utakaposikia tangazo hilo.

**2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia:**

**2.1. Sare ya Shule:**

(a) Sare ya shule hii ni Bluu Bahari iliyopauka, sketi ndefu mpaka chini idadi ya sketi ni mbili na masharti mawili meupe mikono mifupi.
(b) Rangi ya Hijab ni nyeupe na isiyo na urembo wowote, shati mikono mirefu na sketi ndefu.
(c) Viatu vifupi vyeusi vya kamba na soksi ndefu.
(d) Mwanafunzi anaruhusiwa kusuka nywele za kwenda nyuma (twende kilioni) mistari mitano hadi saba. Aidha mwanafunzi haruhusiwi kusukia rasta nyuzi au kuweka dawa. Hatua kali zitachukuliwa kwa yeyote atakayekwenda kinyume na sheria hii.
**N.B:** **<u>Sare za Shule zinapatikana Shuleni</u>**

**3.0. Vifaa vya kujanavyo shuleni:**

1) Ream 1 $A_4$ -photocopy paper (e.g. Nopa au Mondi) Mondi No. 1
2) Ream 1 yenye mistari (ruled paper)
3) Ream 1 ya graph paper

**NB-** Karatasi hizi ni kwa ajili ya mitihani ya wiki, mwezi na mwisho wa muhula kwa mwaka mzima na zitapokelewa katika ofisi ya taaluma.

4) **Vifaa vya usafi:** Wanafunzi wote wanatakiwa kuleta vifaa vya usafi kama ifuatavyo:-
   i) Soft broom na ufagio wa wima wa chelewa na brash ngumu za chooni. Madarasa yatakayoleta ni **KLF na HGK.**
   ii) Mop na ndoo yake na soft broom: Madarasa yatakayoleta ni **EGM, HGE na HGL.**
   iii) Squizer mbili za kudekia na sabuni ya maji/dawa ya chooni (moja ya lita tano) mfano (Tamol ,lit pine , care line )Madarasa yatakayoleta ni **HKL.**
   iv) Mfagio wa wima, Chelewa, Soft broom na Sabuni ya maji (Tamol, lit au Care line): Madara yatakayoleta ni yanayosoma tahasusi

**3.1. Michango mbalimbali**

Ilipwe kwenye akaunti ya shule na mwanafunzi awasilishe risti ya benki.
**Jina la Akaunti**: ZANAKI SECONDARY SCHOOL
**Namba ya Akaunti**: 20301100116 NMB

**(a) Shule za Bweni:**

| Na. | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**(b) Shule za Kutwa:**

| Na. | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa shule | 35,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

(c) Kila katika benki ya NMB.
**Jina la Akaunti**: ZANAKI SECONDARY SCHOOL
**Namba ya Akaunti**: 20301100116 NMB

**4.0 <u>SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE</u>**

Kila mwanafunzi anatakiwa kutii sheria za shule, kuzingatia taratibu zote zilizowekwa pamoja na kufuata maelezo anayopewa na walimu wake.

**4.1 VAZI RASMI LA SHULE**

(a) Kila mwanafunzi atalazimika kuvaa vazi la shule wakati wote anapokuwa katika eneo la shule na nje kwa shughuli za kishule.

(b) Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa vitu vifuatavyo akiwa katika sare ya shule kwa mfano bangili, pete, hereni, mkufu ,leso, 'bronches ' soksi/viatu tofauti na sare ya shule. Vitu hivi vikivaliwa vitanyang'anywa na havitarudishwa.

(c) Mwanafunzi haruhusiwi kupaka hina, wanja 'lip stick', rangi za kucha wala kunyoa nyusi, kutoga pua, kutoga masikio zaidi ya mara moja na urembo wowote.

**4.2 SIMU ZA MKONONI**

Ni marufuku mwanafunzi kuja na simu ya mkononi shuleni au bweni. Endapo kuna jambo la dharula simu ya shule itatumika, akikutwa na simu atanyang'anywa na hatarudishiwa.

**4.3 MAHUDHURIO NA TAALUMA**

(i) Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuwahi shule na darasani. Aidha anatakiwa ahudhurie assembly zote kama ilivyo kwenye ratiba (muda wa kufika shule ni saa 12:30 na assembly huanza saa 1:10 kila siku).

(ii) Mwanafunzi anapaswa kuwa katika eneo la shule wakati wote wa shule na kuhudhuria vipindi vyote. Mwanafunzi anatakiwa kuwa darasani hata kama mwalimu ametoka.

(iii) Ni wajibu wa mwanafunzi kutoa taarifa mapema akiwa amekosa kutimiza mazoezi yoyote au kama amekosa kufanya mitihani.

(iv) Mwanafunzi anapaswa kufanya 'tests' zote au majaribio kama ilivyopangwa katika ratiba.

(v) Mzazi/ Mlezi wasiliana na mwalimu wa darasa kama mtoto wako ana tatizo la kiafya. Utoro shuleni hautavumiliwa.

**4.4. SHUGHULI NYINGINE**

(i) Mwanafunzi atafanya kazi zote za nje ya darasa kwa bidii na kukaa mahali alipopangiwa wakati wote mpaka atakapopewa ruhusa.

(ii) Ni wajibu wa mwanafunzi kuweka mahali pake darasani na bwenini katika hali ya usafi wakati wote na kushiriki katika shughuli zote za usafi wa shule.

**4.5 HESHIMA NA ADABU**

(i) Mwanafunzi anapotoka shule anapaswa kwenda moja kwa moja nyumbani/bweni akiwa amevalia sare ya shule**. *Ni marufuku kuzurura mjini au kusimama ovyo ovyo kwenye kituo cha daladala.***

(ii) Mwanafunzi anatarajiwa kutunza heshima yake wakati wote na kuwa na utii kwa walimu, wazazi na wakubwa zake.

**4.6. WAGENI**

(a) Mwanafunzi haruhusiwi kupokea mgeni wa aina yoyote akiwa shuleni. Mzazi/Mlezi anaweza kumtembelea mwanafunzi lakini lazima kwanza apate kibali cha uongozi wa shule.
(b) Ni mwiko kwa mwanafunzi kuingia shuleni na mgeni yoyote usiku au mchana. Kufanya hivyo kutasababisha mhusika kusimamishwa shule au kufukuza mara moja.

**4.7.MIHULA YA SHULE:**

(i) Kila mwanafunzi lazima afike tarehe iliyopangwa bila kukosa. Haruhusiwi kuondoka kwenda likizo kabla ya tarehe iliyopangwa.
(ii) Wachelewaji watapewa adhabu na kiongozi wa Shule. Hivyo mipango au shughuli zozote za kifamilia zipangwe kwa kutiliwa maanani tarehe za kufunga/kufungua shule.

**4.8 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHWA KUFUKUZWA SHULE:**

(a) Wizi
(b) Uasherati
(c) Kupigana na kupiga
(d) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(e) Kuolewa
(f) Kudharau bendera ya Taifa
(g) Kupata mimba au kutoa mimba ndani ya shule na nje ya shule
(h) Kugoma , kuchochea, kuongoza na kuvuruga amani na usalama wa shule
(i) Kukataa adhabu kwa makusudi au kushawishi wengine kukataa adhabu
(j) Ulevi, uvutaji bangi, na matumizi ya madawa ya kulevya.

**4. 9.** Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na fedha za matibabu au kadi ya bima ya afya. Shule haigharamikii matibabu ya mwanafunzi. Hili ni jukumu la mzazi.

**NB: JITUNZE, JIFUNZE, JIHESHIMU NA ZINGATIA VYEMA SHERIA KWA MANUFAA YAKO.**

**5.0 <u>MAHITAJI MENGINE MUHIMU</u>**

1. Viatu vyeusi vya Kamba (flat) visivyo na visigino
2. Soksi ndefu nyeupe jozi mbili (2) ambazo hazina urembo wowote.
3. Sweta-rangi ya bahari blue kama rangi ya sketi (endapo atahitaji wakati wa baridi). Haruhusiwi kuvaa rangi nyingine, akivaa atanyang’anywa na hatarudishiwa.
4. Madaftari makubwa saba (08) ‘Counter books’.
5. Begi la shule rangi jeusi imara la kuchukulia vitabu na vifaa vingine vya darasani.

6. Vitabu vya kiada - tunashauri mzazi/mlezi ajitahidi kumpatia mtoto wake baadhi ya vitabu atakavyoagizwa afikapo shuleni.

6.0 **VITABU VINAVYOTAKIWA MZAZI KUMNUNULIA MWANAFUNZI**

## A. VITABU VYA JIOGRAFIA KIDATO CHA 5 & 6

**(i)** Practical Geography - by Zisti Kamili

**(ii)** The Earth's Physical Environment (Physical Geograph) by Zisti Kamili

**(iii)** Human and Economic Geography - By Zisti Kamili.

## B. VITABU VYA ADVANCED MATHEMATICS KIDATO CHA 5 & 6

Calculator: CASIO fx-991 E PLOS / CASIO fx-991MS

Books:
1. Pure Advanced Mathematics by J.K. Backhouse
2. Advanced level Pure mathematics by C.J. Tranter
3. Advanced Mathematics book by Septine I.

## C. VITABU VYA BAM KIDATO CHA 5 & 6

Books:
1. Basic Applied Mathematics for Secondary School by Tanzania Institute of Education
2. Basic Applied Mathematics for Secondary School by Septine I.

Calculator: CASIO fx-991 E PLOS / CASIO fx-991MS

## D. VITABU VYA KIINGEREZA KIDATO CHA 5 & 6

Books
i. Advanced learners dictionary
ii. Contemporary English advanced level by Francis Mnyawi
iii.Literature advanced level by Ashed Nicolaus

## E. VITABU VYA KISWAHILI KIDATO CHA 5 & 6

i) Kiswahili Kidato cha 5 & 6 by TET- toleo la 2020 - 21

(i) Fasihi (ii)Lugha na sarufi.

ii)Kamusi ya TUKI.

## F. VITABU VYA FRENCH KIDATO CHA 5 & 6

i) French form 05

ii) Entrain capain 04

iii) On y va 03

iv) French Dictionary

## G. VITABU VYA ECONOMICS KIDATO CHA 5 & 6

(i) Stanlake`s Introductory Economics 7th edition - by S.J Grant

(ii) Principles of Economics - by Ginghan

## H. VITABU VYA HISTORY KIDATO CHA 5 & 6

**(i)** Essentials in History 1 & 2 by Yesen Salehe

(ii) Fundamental Principle of History I & II by Magoti.B

(iii)History paper 1 & 2 by Mwl. Bakari Madaya (2018).

## I. VITABU VYA GENERAL STUDIES KIDATO CHA 5 & 6

**N:B** Wanafunzi wanaochukua tahasusi za masomo ya Chinese, Fineart na Textile maelekezo ya vitabu wanavyotakiwa kununua watayapata wakifika shuleni.

**7.0 USAFIRI**:

Serikali haitagharamia usafiri wa mwanafunzi**. HILI NI JUKUMU LA MZAZI/MLEZI**

**MUHIMU:**

Ni lazima mwanafunzi afike shuleni tarehe iliyopangwa, Shule yetu iko nyuma ya jengo la Umoja wa Vijana (barabara ya Morogoro) jirani na shule ya Sekondari Mzizima na Chuo cha Ufundi Dar es Salaam (DIT).

Mimi pamoja na Jumuiya ya Zanaki tunakupongeza sana kwa kuchaguliwa kujiunga na shule hii. Tunaamini utatoa ushirikiano na mchango katika kuiendeleza Zanaki kielimu na kijamii kwa manufaa yako, shule na Taifa kwa ujumla.

## SHERIA ZA HOSTEL

**(a)** Mwanafunzi huruhusiwi kukaa nje ya eneo la bweni wakati wowote ila kwa ruhusa maalum na kibali cha maandishi.

**(b)** Ruhusa zote zitatolewe na Mkuu wa shule baada ya kupokea maombi ya ruhusa kutoka mama mlezi (Matron), walimu walezi wa hostel au Makamu Mkuu wa Shule ambao watajenga hoja za kuruhusu mwanafunzi atoke. Makamu Mkuu wa shule atatoa ruhusa iwapo Mkuu wa Shule hayupo. Mwanafunzi atakayeondoka Hostel bila kibali, ataondolewa hostel.

**(c)** Wanafunzi wagonjwa watasindikizwa na Matron kwenda hospitali nyakati za usiku. Mwanafunzi haruhusiwi kuondoka kwenda hospitali bila kibali cha matron au uongozi wa shule.

**(d)** Wanafunzi hawaruhusiwi kwenda kwenye sherehe zozote zisizo rasmi, mfano; harusi , kipaimara n.k.

**(e)** Ruhusa maalum itatolewa kwa ajili ya kwenda kwenye msiba wa ndugu wa karibu tu, na kwa muda usiozidi siku tatu.

**(f)** Kutakuwa na ‘Roll Call’ kila siku saa 12:30 jioni na usiku. Aidha, matron anaweza kuitisha ‘roll call’ wakati wowote ule baada ya masomo ya jioni.

**(g)** Matibabu maalum sharti yaandikishwe shuleni ili matron awe na taarifa. Mwanafunzi kuleta vyeti vinavyohusika kutoka kwa daktari.

**(h)** Hairuhusiwi kulala wanafunzi wawili kitanda kimoja. Endapo utakutwa umekiuka sheria hii utaondolewa hosteli.

**CHAKULA**:

(a) Chakula chote kitaliwa ndani ya bwalo la shule. Wanafunzi hawaruhusiwi kula bwenini.

(b) Mwanafunzi yeyote hataruhusiwa kuingia jikoni ila tu kama amepangiwa zamu huko.

**LIKIZO FUPI (MID TERM)**

Mwanafunzi haruhusiwi kwenda likizo fupi (mid term) kwa ndugu/rafiki yeyote isipokuwa kwa kibali cha mzazi/mlezi. Kibali kitamke wazi, mwanafunzi aruhusiwe kwenda kwa nani na

anwani ya mtu huyu ieleweke wazi kuwa jamaa aliyeruhusiwa atatakiwa yeye binafsi kufika shuleni kumchukua mwanafunzi anayehusika.

**WAGENI**

(a) Wageni wasioorodheshwa kwenye fomu ya kujiunga na shule, hawaruhusiwi kabisa kuwatembelea wanafunzi.
(b) Ni mwiko kwa mwanafunzi kuingia shuleni na mgeni yeyote usiku au mchana. Kufanya hivyo kutasababisha mhusika kusimamishwa shule au kufukuzwa mara moja.

**USALAMA/USAFI BWENINI**

(a) Kila mwanafunzi anapaswa kuweka vitu vyake vizuri na kwa unadhifu na usalama. Masanduku yote yawe na funguo. Vifaa vyote vinavyoshawishi wizi visiletwe shuleni mfano; radio, simu za mikononi, vito vya thamani (mikufu, herein n.k). fedha za matibabu kwa wanafunzi wa hostel wazitunze vizuri ili ziwasaidie wanapougua wakiwa shuleni.

(b) Ni marufuku kuweka vitu vinavyohatarisha maisha/afya ya binadamu bwenini kwa mfano kisu n.k.
(c) Kila mwanafunzi anawajibu wa kutunza mazingira na usafi wa bweni.

**SALA**

Sala za kabla ya kulala ziwe fupi na zifanyike baada ya kumaliza kusoma saa 4:30 usiku. Sala za alfajiri zitafanyika kwa taratibu zisiwasumbue wengine. Baada ya sala ya usiku, kila mwanafunzi atatakiwa kuwa kitandani kwake ifikapo saa 4:45 usiku, na taa zote zitazimwa na viongozi wa kila bweni.

**MATIBABU**

Shule inatoa huduma ya kwanza pale hostel. Kama mwanafunzi atakuwa na tatizo kubwa, itamlazimu kupata matibabu nje ya shule katika hospitali ya jirani na shule. Hivyo mzazi unatakiwa kumpatia mtoto wako fedha ya kujitibia na kama ana kadi ya bima ya afya tafadhali mpatie aje nayo.

KARIBU SANA!

________________________

**MKUU WA SHULE**
**D.B. KOKA**
**0756475424**

***Iletwe siku ya kufungua shule ikiwa imejazwa kikamilifu.***

1. Jina lako ………………………………………………………… ***Picha ya Mwanafunzi***
2. Tarehe ya kuzaliwa ……………..……………………..........
3. Dini/dhehebu …………………………………………..........

4. Majina ya Wazazi ***Picha ya Baba*** ***Picha ya Mama***

   (a) Baba ……………………………………….

   (b) Mama ………………………………………

   (c) Yatima/siyo yatima. Eleza………………......

   ……………………………………………….

5. Jina la Mlezi [kama huna mzazi]

   (a) ……………………………………………………………………………………

   (b) Uhusiano wako na Mlezi …………………………………………………………...

   **NB:** Picha ya Mlezi [kama huna Mzazi]

6. Una ndugu wangapi? [Ujihesabu] ……………………………………………………..
   (a) Idadi ya ndugu (i) Dada ……………………………..
   (ii) Kaka ……………………………..
   (b) Wewe ni wangapi kuzaliwa? …………………………

7. Umbali kutoka shuleni hadi unapoishi (kilomita ngapi?)………………………………………….

8. (a) Je, unatumia usafiri wa maji?

   Ndiyo/Hapana (kata ambayo haiitajiki).

   (c) Kama Ndiyo, umetoka wapi?.......................................................................................

**9.** (a**) Kazi ya baba/mlezi**

……………………………………………

Anwani yake

……………………………………………

……………………………………………

……………………………………………

……………………………………………

Simu……………………………………

**(b) Kazi ya mama/mlezi**

……………………………………………

Anwani yake

……………………………………………

……………………………………………

……………………………………………

……………………………………………

Simu ……………………………………...

10. Mahali Mzazi/Mlezi anapoishi

Mtaa ……………………………………………Eneo ……………………………………………

Namba ya nyumba ……………………………...Simu ……………………………………………...

11. Jina la ndugu wa karibu

…………………………………………………………………………………………………...

Kazi yake……………………………………Anapoishi………………………………………..

Namba ya nyumba……………………………..Eneo……………………………………………..

Simu……………………………………………Uhusiano na ndugu huyo [eleza] ………………….

…………………………………………………………………………………………………...

12. Michezo anayopenda/anayocheza mwanafunzi

(i) ……………………………………………………………………………………………..

(ii) …………………………………………………………………………………………......

(iii) ……………………………………………………………………………………………..

13. Maoni/Maelezo ya mzazi/mlezi

……………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………..

14. Mwanafunzi atakaporipoti shuleni anatakiwa kuja na nakala ya :-

(i) Cheti cha kuzaliwa.

(ii) Result Slip.

- ***Taarifa iletwe mapema shuleni linapotokea badiliko la anwani.***

**UTHIBITISHO WA KUKUBALI NAFASI**

1. Mimi ……………………………………………………………….kidato cha ……………...
   Nimesoma na kuzielewa sheria na taratibu za Shule ya sekondari Zanaki. Naahidi kuwa nitatimiza sheria zote kwa kadiri ya uwezo wangu. Nakubali nikivaa nguo au mapambo yasiyoruhusiwa vichukuliwe na shule na nisirudishiwe.


   **Sahihi** ……………………………………**Tarehe** ………………………………………..

2. Mimi ……………………………………………[Mzazi/Mlezi] wa ………………………..
   Nimezisoma na kuzielewa sheria na taratibu za shule. Naahidi kushirikiana na walimu katika kumhimiza mwanangu kufuata maagizo yote ya shule.

   **Sahihi** ……………………………………**Tarehe** ………………………………………..

**SHULE YA SEKONDARI ZANAKI**

**<u>MSHONO WA SKETI YA MWANAFUNZI</u>**




**NB: (i)** Mshono wa sketi ni **<u>" A" shape</u>** na siyo "Solo" au "Tight"

(ii) Urefu wa sketi kwa wasiovaa hijabu ni **sentimita tatu** kutoka kwenye magoti.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**STATION:** *ZANAKI SECONDARY SCHOOL-ILALA*

**DATE**: …………………………………………………..

**PART A:**

TO: ……………………………………………

Medical Officer

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………….

Miss/Mr …………………………………………………………………………………….

Please examine the above named to his/her fitness for admission as a student in the following common disease/problems:-

Put tick ( √ ) for positive and a cross ( X ) for a negative against in a box provided.

| | |
|---|---|
| Pregnance | |
| Asthma | |
| Sight | |
| Diabets | |
| Worm (stool) | |
| Epilepsy | |
| TB (Tuberculosis | |
| Sickle cell | |
| Heart disease | |
| Yellow fever | |
| U.T.I | |
| Malaria | |
| | |
| | |
| | |

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physically **FIT/UNFIT** for admission as above.

**Date………………………………………………Signature……………………………….**

**Station …………………………………………...Designation ……………………………**

## MAHITAJI YAO

(A) **Matresses:**

(1)Godoro la sponge - 2 ½ ft X 6 ft
(2)Mashuka jozi mbili rangi ya pink
(3)Mto mmoja na foronya mbili ya pink
(4)Bed cover isiyo na urembo rangi ya pink
(5)Chandarua cheupe

(B) **Vifaa vya bafuni na usafi**

(1)Ndoo ya plastic yenye mfuniko
(2)Kandambili pea moja (1)za kawaida plastic
(3) Taulo moja (1)
(4) Soap dish
(5) Vibanio vya nguo 12
(6)Tochi (1)

(C)**Nguo za kuvaa weekend na weekday**:
Sketi nyeusi ndefu box rinda na blauzi ya zambarau (puple) pea mbili (02)
(zinapatikana shuleni)

(D) **Nguo za kushindia:**
(1) Kanga/kitenge pair moja (1) na pair ya pili kwa wanafunzi waiislam
(2) Nguo za ndani za kutosha pair 5 (tano)
(3) Taulo za special (padi) paketi 4 au Zaidi kwa term
(4) T-shirt 2 rangi ya zambarau
(5) Track suit daki blue mbili i zisizobana (ziwasaidie kuzuia mbu wa usiku wakisoma .
(6) Sandles
(7) Mwamvuli
(8) Begi moja la madaftari na vitabu vya shule.
(9) Soksi nyeupe pair 4
(10)Kapeti la meza mita moja rangi yoyote.

(E) Vyombo vya kuweka chakula/chai
(i)Sahani
(ii)Kijiko
(iii)Kikombe

**Angalizo**: Nguo za nyumbani haziruhusiwi, ukija nazo utanyang'anywa na hutarudishiwa.